

# ASIREGEE MOYOWE

## Ijumaa Kuu-Mateso ya Bwana

Na. Miyombo. G. A  
 Makere- Kigoma  
 Machi, 2005

**♩ = 90**

**Piano**

1. A si re ge e mo yo we a si to ke ma cho zi,  
 A kim ku mbu ka Mu ngu we kwa ya ke ma ko mbo zi

**Pno.**

mtu a ro ho msa la ba ni mta ka ku fa mwe nye we

**Piano**

kwa sa ba bu kum - pe nda ni na ni - mfu nga mo yo we.

2. Bustani mle Getsmani, amwomba Mungu Baba.  
 Je, Mungu-mtu ana nini! nguvu zake ni haba.  
 Bwana wangu waziona, dhambi za binadamu,  
 Mwili wake umetona, kama jasho la damu.

3. "Salamu Rabbi, Salamu", anena Yuda mbaya.  
 Mwenye moyo wake mgumu, ambusu pasi haya.  
 Aliwambia basi, "ntakayembusu ndiye",  
 Mtwani na kwa upesi, Yuda nani? Ni sie.

4. Yuda nani? siye yeye, aliyetenda dhambi.  
 Tukimkosa Mungu Baba, kumdharau na Mwana.  
 Tukimsikitisha roho, tu vipofu kama Yuda,  
 Tunatupa neema yake, itokayo kwa kwa Yesu.

5. Wote ni kupiga mbi, mitume we pamoja.  
 Wamtia mikono yao, askari walokuja.  
 Wampeleka hukumuni, aamuliwe na watu,  
 M'nye kutoka uwinguni, mwamuzi mkuu wa watu.

6. Mtume Petro akanusha, amenena simjui.  
 Uhodari umekwisha, machowe hainui.  
 Pilato amwona Rabbi, hakukosa 'ta neno,  
 Asema "Sioni dhambi", lakini ni mwoga mno.

7. Hathubutu kumwachia, si hukumu aomba.  
 "Mmoja nitamfungulia, Yesu au Baraba".  
 Wayahudi mwamtukana: "Baraba aachiwe,  
 Yesu afe msalabani, damuye juu yenu".

8. Pilati, hukumu gani, "simo nanawe mkono.  
 Mkimtaka Yesu mwueni", la mwanzi hilo neno?  
 Mara askari wamwanza, na kupiga kelele,  
 Kumcheka na kumchokoza, mwenye mema milele.